OFISI YA RAIS –TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI.

**SHULE YA SEKONDARI IRKISALE,**
**S.L.P 68,**
**MONDULI.**
**TAREHE……/..…/2024.**

**KUMB.NA IRK./SS/WAZ/GF/J.I/ 2024/18.**

**JINA LA MWANAFUNZI…………………………….........................................…………………………**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IRKISALE WILAYA YA MONDULI MKOA WA ARUSHA MWAKA 2024.**

1.0 Ninafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza mwaka 2024** katika **Shule ya Sekondari IRKISALE** iliyopo Wilaya ya Monduli Mkoa wa Arusha, Makao makuu ya Kata ya Lolkisale, Kijiji cha Lolkisale kilomita 65 kutoka Monduli Mjini.

Usafiri wa kufika Shuleni unapatikana kwa urahisi katika Mji mdogo maarufu kwa jina la **DUKA BOVU** , Mji ulioko katika barabara kuu iendayo Dodoma karibu na njia panda ya kwenda Monduli mjini.Nauli ni Sh.5000/= toka **DUKA BOVU** hadi shuleni. Ingawa inaweza kubadilika wakati wowote kulingana na hali ya hewa. Shule hii ni ya mchanganyiko wa Wavulana na Wasichana na Wanafunzi wote hulala Bweni.Shule ipo katika mazingira yanayoshawishi mwanafunzi kusoma kwa bidii, hivyo ona fahari kupata nafasi hii adimu.

- Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **08/01/2024.**
- Unatakiwa kuripoti tarehe **08/01/2024** siku ya Jumatatu. Ni vema kuwahi Dukabovu saa nne asubuhi.
- Unatakiwa kuripoti Shuleni ndani ya wiki mbili tangu shule kufunguliwa.Hivyo tarehe ya mwisho ya kuripoti ni tarehe **15/01/2024.**
- Mwanafunzi asiporipoti hadi tarehe ya mwisho ya kuripoti yaani **15/01/2024** hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Mzazi/Mlezi wake ikiwa ni pamoja na kukamatwa na polisi na kushtakiwa mahakamani.
- Mzazi atakayempeleka mtoto wake Shule ya binafsi **(Private School)** atoe taarifa kwa Afisa ElimuWilaya au Mtendaji wake wa Kata au Afisa Elimu wake wa Kata au Mkuu wa shule akitaja jina la Shule na Wilaya Shule ilipo.

2.0 Mambo muhimu unayotakiwa kuzingatia na kuyatimiza kabla au siku ya kufika Shuleni ni kama yafuatayo:-

**2.1 SARE ZA SHULE**

**A. WASICHANA:**

i. Sketi mbili (02) rangi ***KIJANI KIBICHI (CRETA)*** ndefu. Sketi iwe ndefu toka kwenye kitovu hadi chini ya kisigino

***Kitambaa kiwe kizito gredi 1 mshono wa marinda.***

ii. Suruali mbili (02) rangi ***KIJANI KIBICHI (CRETA),*** isiyo ya mlegezo na mifuko isiwe ya kubandika.

**Suruali ni lazima kwa wasichana wote**.

***iii.*** Shati mbili (02) nyeupe tetron mikono mifupi na kwa ***wasichana wa Kiislamu tu, mashati yawe meupe ya mikono mirefu.***

iv. Soksi ndefu jozi mbili (02) nyeupe kwa wasichana

v. Sweta rangi ***KIJANI KIBICHI*** yenye shingo ya **"V"**

vi. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili.

vii. Shuka mbili (02) *rangi ya* ***PINKI.***

*viii.* Tai moja (01) rangi ***KIJANI*** **au** ***KIJANI*** **yenye mistari** ***MEUPE.***

ix. ***Kitenge au kanga kipande kimoja (1) kwa ajili ya kuogea.***

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**
**SHULE YA SEKONDARI IRKISALE**
**TAARIFA YA MWANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024.**

1. **Shule ya Sekondari……………………………………………………………………………….**

2. Shule ya Msingi aliyotoka………………………………………………………………….

3. Jina la mwanafunzi…………………………………………………….Jinsia **ME** ☐ **KE** ☐

4. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………

5. Kijiji atokacho……………………………………………………………………………………

6. Kata atokayo………………………………………………………………………………………

7. Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa atokako………………………………………………………
   Namba ya Simu ……………………………………………………………………………………

8. Jina la Balozi atokako…………………………………………………………………… ……..
   Namba ya Simu …………………………………………………………………………………

9. Jina la Baba/Mlezi……………………………………………………………………………
10. Namba ya Simu…………………………………………………………………………………

11. Jina la Mama/Mlezi………………………………………………………………………………

    Namba ya Simu ……………………………………………………………………………………

12. Jina la Ndugu wa karibu
    i. Jina ……………………………………………………………………………………… Namba ya Simu …………………………………………………………………………
    ii. Jina ……………………………………………………………………………………… .Namba ya Simu …………………………………………………………………………
    iii. Jina ……………………………………………………………………………………… Namba ya Simu ……………………………………………………………………………

**Ninathibitisha kuwa tarifa zilizojazwa hapo juu ni sahihi**

Jina…………………………………………………. Saini………………… Tarehe………………………

Jina la Mwalimu wa Darasa…………………………… Saini…………. Tarehe ………………




***Mkuu wa Shule***

**NGUO ZA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) NA MICHEZO:**

i. Sketi mbili (02) rangi ya ***BULUU BAHARI*** mshono wa marinda.
ii. T shirt rangi ya ***KIJANI KIBICHI*** shingo ya mviringo isiyo ya maandishi ya aina yeyote.
iii. Traki suti rangi ***KIJANI KIBICHI*** isiyo na maandishi yeyote kwa ajili ya michezo.
iv. Raba kwa ajili ya michezo.

**MUHIMU:**

- ***Ifahamike wazi kuwa mwanafunzi atavaa sare ya shule au shamba dress wakati wote awapo shuleni.Mavazi mengine yoyote hayaruhusiwi. Kwa hiyo yasiletwe kabisa shuleni.***
- ***Hakikisha umeweka alama ya jina lako kwenye sare, Nguo, Daftari, Vitabu na vifaa vyako vyote.***
- ***Kwa wasichana wa Kiislamu wawe na Shungi mbili (02) Ndefu nyeupe na mashati meupe tetroni mikono mirefu na shungi ya kushindia ni rangi ya njano.***

**B. WAVULANA:**

i. Suruali mbili (02) rangi ***KIJANI KIBICHI (CRETA)*** isiyobana, isiyo ya mlegezo na mifuko isiyo ya kubandika na **kitambaa kiwe kizito gredi 1**.
ii. Shati mbili (02) nyeupe tetroni mikono mifupi.
iii. Soksi ya rangi ***KIJIVU*** ndefu jozi mbili (02).
iv. Sweta rangi ya yenye shingo ya"V"
v. Viatu vyeusi jozi mbili(02) vya kufunga na kamba
vi. Mkanda mweusi wa ngozi.
*vii.* Shuka mbili (02) rangi ya ***BULUU BAHARI***.
viii. Tai moja (01) rangi ***KIJANI*** *au* ***KIJANI*** *yenye mistari* ***MEUPE.***

**NGUO ZA KUSHINDIA NA MICHEZO:**

i. Suruali mbili (02) rangi ya ***BLUU BAHARI*** isiyobana, isiyo ya mlegezo na mifuko isiyo ya kubandika.
ii. T- shirt rangi ya ***KIJANI*** shingo ya mviringo isiyo na maandishi ya aina yeyote ile.
iii. Traki suti rangi ***KIJANI*** isiyo na maandishi yeyote kwa ajili ya michezo.
iv. Raba kwa ajili ya michezo.
v. Taulo ya kuogea
vi. Bukta kwa ajili ya michezo rangi ya njano au buluu.

**MUHIMU:**

- ***Ifahamike wazi kuwa mwanafunzi atavaa sare ya shule au shamba dress wakati wote awapo shuleni. Mavazi mengine yoyote hayaruhusiwi. Kwahiyo yasiletwe kabisa shuleni.***
- ***Hakikisha umeweka alama ya jina lako kwenye sare, Nguo, Daftari,Vitabu na vifaa vyako vyote.***

**2.2VIFAA NA MAHITAJI MENGINE BINAFSI KWA WASICHANA NA WAVULANA.**

i. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ (upana) kwa futi 6(urefu)
ii. Ndoo 1 ya kuogea na kufulia lita 10.
iii. Sanduku la chuma/bati lenye kufunga kwa kofuli.
iv. **Daftari kubwa "(counter book Quire3**)" 12, kalamu, rula, penseli na Mathematical set(kompasi)
v. Sahani, bakuli, kijiko na kikombe (ni vema sahani na bakuli viwe vya chuma/bati).
vi. Toilet paper (kwa matumizi ya chooni) tano(5)
vii. Sabuni ya kutosha kwa ajili ya kufulia na kuoga.
viii. Rangi ya viatu (dawa ya viatu) nyeusi na brashi yake.
ix. Begi imara kwa ajili ya madaftari na vitabu vyake.
x. Dawa ya meno na mswaki.
xi. Mafuta ya kujipaka anayotumia mwanafunzi
xii. Neti moja (01) kwa ajili ya kujikinga na mbu.Ni vema rangi iwe ya kijani au bluu.
xiii. Nauli ya kutosha kufika shuleni na kurudi wakati wa likizo.
xiv. **Student Oxford English Dictionary** (English-English) kwa ajili ya kujifunza lugha ya Kiingereza.
xv. Kamusi ya Kiswahili sanifu (Kiswahili-Kiswahili)
xvi. Blanketi moja (01) la kawaida.
xvii. Tochi 1
xviii. **Rimu moja A4** kwa ajili ya mitihani na majaribio ya kila wiki
xix. Jembe na Fagio au chelewa kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule.
xx. Mchango wa maji Tsh.2000/= uliopitishwa na wazazi na utapokelewa na Mwenyekiti wa maji ( Mzazi Mwakilishi)

2.3 Mwanafunzi akiugua awapo shuleni, Shule itampa huduma ya kwanza na kumpeleka kituo cha afya Lolkisale na endapo atahitajika kupelekwa nje ya Lolkisale kwa matibabu gharama za matibabu mzazi atahusika.Pia mzazi unashauriwa kumkatia mtoto wako **Bima ya Afya** iliyoboresha ambayo ni **Tsh 6000/=** kwa mwaka huduma hii itapatikana kituo cha afya Lolkisale.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamina ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais –Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini.

**Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo utafafanuliwa zaidi ukifika shuleni.**

i. Kuheshimu Viongozi, Wazazi Wafanyakazi wote, Wanafunzi na jamii inayotuzunguka.
ii. Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na shughuli zote za ndani na nje ya shule.
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni "(preparations)"
iv. Kuwahi katika shughuli zote za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kuifahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo kwa wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa kauli, mwili, mavazi, mali yako binafsi, mali ya Shule na mazingira.
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapokuwa Shule au utokapo nje ya Shule kwa kibali maalumu.
viii. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote uwapo shuleni.
ix. Kutunza mali za Umma na mali binafsi
x. Huruhusiwi kumiliki au kutumia simu uwapo Shuleni pasipo idhini maalumu.
xi. Huruhusiwi kutoka nje ya Shule bila kibali kinachoonesha unakokwenda na muda wa kurudi.
xii. Huruhusiwi kutumia vifaa vya umeme bwenini au darasani mfano: pasi, heater n.k.
xiii. Unapaswa kupanga mstari wakati wa kupokea huduma ya chakula jikoni.

xiv. Ni marufuku kuingia jikoni bila idhini ya wahusika.
xv. Ni marufuku kutumia lugha ya matusi kwa mtu yeyote mahali popote.

**3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule.**

i. Wizi wa aina yeyote ndani na nje ya shule.
ii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi, sigara n.k
iii. Kupigana au kupiga ndani au nje ya shule.
iv. Kuharibu kwa makusudi mali ya mtu,shule, Umma na fedha za Serikali.
v. Kudharau Bendera ya Taifa ,Viongozi wa Serikali, walimu na walezi wengine shuleni.
vi. Kuoa na kuolewa au kufanya mapenzi shuleni au kuwa na mahusiano ya kimapenzi shuleni au nje ya shule.
vii. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya Shule.
viii. Kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba ndani na nje ya shule.
ix. Kutohudhuria vipindi vya darasani ikiwa ni pamoja na vipindi viwili vya dini kila wiki, kutofanya mitihani, majaribio au kulala bwenini bila ruhusa maalumu au kazi nyingine za shule bila kibali cha Mkuu wa Shule.
x. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa Shule, raia na mali zao.
xi. Kukataa adhabu makusudi au kupigana au kumpiga mwalimu.
xii. Kuvunja sheria na taratibu za Shule kwa makusudi.
xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi hairuhusiwi kabisa
xiv. Makosa ya jinai.
xv. Utoro Shuleni kwa siku tisini (90) mfululizo pasipo taarifa rasmi au kutoroka usiku au mchana.
xvi. Mvulana kwenda kulala bweni la wasichana, au msichana kwenda kulala bweni la wavulana.
xvii. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja (**Ushoga**).

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

i. Medical Examination form iliyoambatanishwa ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali baada ya kukupima na uikabidhi kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.
ii. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi.
iii. Fomu ya mzazi na Mwanafunzi kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kwa ukamilifu.Uongozi wa Shule hautapenda kuona usumbufu wowote unaotokana na kutozingatia na kutotimiza maelekezo haya.**

*Kwa maelekezo zaidi wasiliana na yeyote kati ya wafuatao:*

- **Mkuu wa Shule -0754 852 169/0785774235**
- **Makamu Mkuu wa Shule -0759616161**
- **Mwalimu wa Malezi -0756331865**
- **Mwalimu wa Malezi -0758446665**

***"ELIMU KWA MAENDELEO"***

**KARIBU IRKISALE**




**MKUU WA SHULE.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**

**SHULE YA SEKONDARI IRKISALE**

**S.L.P 68 MONDULI**

# HATI YA UTII WA SHERIA

**A:SEHEMU YA MZAZI**

Mimi Bw/Bibi ………………………………………………………………………


Nimesoma kwa makini sheria za Shule kama zilivyoandikwa katikka barua ya kujiunga na shule na nikakubaliana nazo, Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kuhakikisjha kuwa mwanangu anazifuata kikamilifu kwa manufaa ya Umma.

**Saini ya Mzazi/ Mlezi………………………………**

**B: SEHEMU YA MWANAFUNZI.**
Mimi………………………………………………………………………………………
Motto wa Bw/Bibi…………………………………………………………………
Nimesoma kwa makinni sheria za Shule kama zilivyoandikwa na nimezikubali sheria hizo. Ninaahidi kuzifuata na kuzitii nikijua dhahiri kuwa ninaelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma

**Saini ya Mwanafunzi……………………………………**

**Tarehe……………………**



# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA MONDULI

# SHULE YA SEKONDARI IRKISALE

# MEDICAL EXAMINATION FORM

Student's full name: ..........................................................................................

Age: ...................................................... Sex......................................................

Blood count (Red and White): ..............................................................................

Stool examination: .................................................................................................

Urine analysis: ......................................................................................................

Syphilis test: ..........................................................................................................

Eye test: ................................................................................................................

TB test: .................................................................................................................

Eat test: ................................................................................................................

Chest: ...................................................................................................................

Liver: ....................................................................................................................

Abdomen: ..............................................................................................................

Any other physical defect/ impairment.
..........................................................................................................................


..........................................................................................................................

Date...........................................................

Signature....................................................

Designation...............................................

Station....................................................  **Official Stamp**




**Head of School.**